Adhama ni neno lenye maana ya "Uzuri wa hali ya juu sana". Na huu uzuri ni Bwana Yesu tu peke yake ndio anao, yeye ndiye mwenye adhama.

> *Zaburi 93: 1 "Bwana ametamalaki, amejivika adhama, Bwana amejivika, na kujikaza nguvu. Naam, ulimwengu umethibitika usitikisike;*
>
> *2 Kiti chako kimekuwa thabiti tokea zamani; Wewe ndiwe uliye tangu milele"*

Mistari mingine michache inayozungumzia adhama ni kama ifuatayo..

> *Zaburi 96:6 "Heshima na adhama ziko mbele zake, Nguvu na uzuri zimo katika patakatifu pake".*

> *Zaburi 104:1 " Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Wewe, Bwana, Mungu wangu, Umejifanya mkuu sana; Umejivika heshima na adhama.*

> *2 Umejivika nuru kama vazi; Umezitandika mbingu kama pazia;"*

> *Isaya 33:21 " Bali huko Bwana atakuwa pamoja nasi, mwenye adhama; mahali penye mito mipana na vijito, pasipopita mashua na makasia yake; wala hapana merikebu ya vita itakayopita hapo".*

> *2Wakorintho 4:7 "Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu".*

Mistari mingine iliyotaja neno hilo ni pamoja na *1Nyakati 16:27, Zaburi 21:5, Zaburi 113:3,  Zaburi 148:13 na Zaburi 29:4.*

Hivyo Bwana Yesu, peke yake ndiye mwenye heshima yote na adhama yote, na wala hakuna mwingine.

> *Ufunuo 5:9 "Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa*

> *ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa"*

Maran atha!

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

pia kama utapenda uyapate mafundisho haya kwa njia ya Whatsapp au email basi tutumie ujumbe kwenye namba hizo hizo.

---

Mada Nyinginezo:

> *Mpumbavu ni nani katika biblia? (Zaburi 14:1, Mithali 10:14)*

> *KITABU CHA YUDA: SEHEMU YA 3*

> *VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 10 (Kitabu cha Zaburi).*

> *Nini maana ya..“wakiwazuia watu wasioe” (1Timotheo 4:1)*

> *UTUKUFU NA HESHIMA.*

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp